BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukuwani, Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA AFYA ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,**

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kutujaalia uzima na afya njema tukaweza kukutana tena katika Baraza hili la Kumi na Mbili kwa ajili ya kuendelea kuwatumikia wananchi wetu. Aidha, nikushukuru na kukupongeza Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza Baraza hili tukufu, ni imani yetu kwamba utaendelea kuliongoza Baraza hili kwa uadilifu wa hali ya juu na kuimarisha Demokrasia katika chombo hichi muhimu cha wananchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kiupekee kabisa, nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kuweza kuiboresha huduma ya Afya nchini kwa kujenga Hospitali za Wilaya, Mkoa na pamoja na kuboresha mifumo ya utoaji huduma, madawa Hospitalini na vitendea kazi sambamba na kuanzisha huduma ya Bima ya Afya nchini.

Pia niwapongeze wasaidizi wake Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili Mheshimiwa

Hemed Suleiman Abdulla kwa kumsaidia vyema Mhe. Rais wetu katika kutekeleza majukumu yake kwa maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Wawakilishi wote waliomo katika Baraza lako Tukufu kwani kuchaguliwa kwetu kuja kuwawakilisha wananchi, ni wazi kwamba wananchi wamejenga imani kubwa kwetu, nasi ahadi yetu kwao ni kwamba tutawatumikia kwa dhati kama ambavyo walivyotuamini kutuleta katika chombo hichi kwa lengo la kutetea maslahi yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Sina budi pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Afya pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara hii kwa mashirikiano waliyotupatia kamati wakati wa kupitia Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii.

Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yetu kwa umoja wao na kazi nzuri waliyoifanya kiasi cha kunirahisishia kazi ya kuongoza kikao kuwa nyepesi na ya ufanisi. Kwa kweli, ni wajumbe Mahiri, ambao wameweza kuijadili kwa kina na ipasavyo makadirio hayo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinisha zinatumiwa kwa matumizi yaliokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa heshima napenda kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama hivi ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Sabiha Filfil Thani | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira) | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Abadalla Hussein Kombo | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Haji Omar Kheir | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Sulubu Kidongo Amour | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Salma Mussa Bilali | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Bahati Khamis Kombo | Mjumbe |

Aidha, Kamati yetu inafanyakazi na makatibu watatu (3) ambao wamekuwa wakitusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu, makatibu hao ni:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Ndg. Talib Enzi Talib | Katibu |
| *2.* | Ndg. Bakar Makame Haji | Katibu |
| *3.* | Ndg. Salha Abdulla Abdulla | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,**

Miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati yetu ni kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Wizara husika ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka, hivyo katika kutekeleza jukumu hilo lililoelezwa katika Kanuni ya 107(3) Kamati ilikaa na kujadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Wizara ya Afya na leo hii kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati nawasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Bajeti hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha **2024/2025** ina Mafungu **mawili (2),** ambapo **Fungu H01 Wizara ya Afya** na limepanga kutekeleza Programu Kuu Tatu (3) zenye Programu Ndogo Saba **(7)** ambapo kwa ujumla fedha zilizoombwa kwa Wizara ya Afya ni **Shilingi Bilioni 282,756,472,000/=** ambapo Makadirio ya Mapato yatakayokusanywa kwa **Fungu HO1 ni Shilingi Bilioni 3,719,683,000/=**

**Fungu HO2 Hospitali ya Mnazi Mmoja** imepanga kutekeleza Programu Kuu Mbili (2) zenye Programu Ndogo Tano (3) ambapo zimeombwa jumla ya **Shilingi Bilioni 61,329,600,000/=** ambapo Makadirio ya Mapato yatakayokusanywa kwa **Fungu HO2 ni Shilingi Bilioni 1,339,086,000/=**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imebaini kuwepo kwa ongezeko kubwa na kupungua kwa makadirio kwa baadhi ya vifungu katika Programu Kuu mbali mbali pamoja na huduma zake (**HO1 na H02).** Kamati ilipohoji iliarifiwa kuwa hali hiyo imetokana na kuongezeka kwa baadhi ya Huduma katika Programu Kuu husika ambazo kabla hazikuwepo. Pili, ni kutokana na baadhi ya huduma kuunganishwa na huduma nyengine na tatu, ni kuongezeka kwa Miradi pamoja na Wafadhili. Mfano; Huduma ya Uratibu na Uendeshaji wa Shughuli za Kinga Pemba (**HH01010119)**, Huduma ya Elimu ya Afya kwa Jamii (**HH01010105**) na Huduma za Ufuatiliaji wa Maradhi ya kuambukiza (Progaramu ya Ukimwi na Malaria) **HH01010114**.

## FUNGU H01 WIZARA YA AFYA

**Mheshimiwa Spika,**

Miongoni mwa njia moja wapo ya kuiongezea mapato Serikali ni kusajili vituo vya Afya vilivyopo nchini, hivyo Kamati inaishauri Wizara kuwa na utaratibu wa kuvifuatilia na kuvisajili vituo ambavyo bado havijasajiliwa, hasa vituo binafsi vinavotoa huduma za matibabu ya afya vilivyopo Mahotelini, kwani Kamati imebaini kuwa kumekuwa na vituo vingi ambavyo vikipatiwa utaratibu na kusajiliwa basi vitaongeza mapato Serikalini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inashauri kuanzishwa Sheria itakayowezesha Mabwana Afya katika Baraza la Mazingira kuwa na uwezo wa kuwachukulia hatua watakaobainika kuhatarisha afya katika jamii ikiwemo kuwatoza fidia ya papo kwa papo itakayowezesha kuongezeka kwa eneo jengine la mapato litokanalo na usimamizi wa Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,**

Kuhusu huduma ya utoaji wa damu salama kwa wagonjwa, Kamati inashauri Hospitali binafsi kuchangia malipo kwa ajili ya kupatiwa huduma hiyo na Wizara kuzifuatilia kwa kuzikagua hospitali hizo ili kuhakikisha huduma hiyo haitolewi kwa bei ya juu kwa wananchi. Pia Kamati inashauri fedha itakayochangiwa kwa huduma za damu kutoka Hospitali Binafsi zibakie kwenye kitengo cha damu ili kusaidia baadhi ya huduma zinazotolewa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya Fedha kupitia Kitengo cha Bajeti kukaa na Wizara husika ili kupanga makadiro yanayoendana na Uhalisia, kwani Kamati imebaini kuna baadhi ya maeneo ya makadirio ni makubwa wakati uhalisia wa makusanyo ni mdogo, na baadhi ya maeneo makadirio ni madogo wakati uhalisia wa makusanyo ni makubwa. Hivyo, Kamati imeona kuwa vifungu vyenye makadirio madogo kuna haja ya kupangiwa makadirio zaidi ili kuenda sambamba na uhalisia wa makusanyo.

## PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0101)

**Mheshimiwa Spika,**

Lengo la Programu hii ni kutoa elimu ya Afya kwa jamii ya jinsi gani tunaweza kujikinga juu ya maradhi yanayoambukiza na yasiyoambukiza pamoja na kutoa elimu juu ya maradhi ya mripuko.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imebaini kuwa makadirio ya matumizi ya Program ndogo ya **SH010101** yameongezeka kutoka shilingi Bilioni **36,898,364,000** kwa mwaka 2023/2024 hadi kufikia Bilioni **100,819,301,000** kwa mwaka 2024/2025. Kamati imearifiwa kuwa ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa Miradi ya Maendeleo. Mfano; Mradi wa Ukarabati wa vituo vya afya na Mradi wa Huduma za ufuatiliaji wa maradhi ya kuambukiza. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuwashirikisha ipasavyo wataalamu tokea mwanzoni mwa Miradi ili kuhakikisha kuwa Miradi hiyo inafikiwa malengo yalikusudiwa kwa mujibu wa thamani ya fedha.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara kwa kujenga hoja Serikalini na kupatiwa vifungu vya matumizi, ambavyo kwa mwaka wa fedha uliopita havikuweza kukadiriwa fedha za matumizi; Huduma za Afya ya jamii (**HH01010122)** ambapo itasaidia kuimarika kwa huduma za afya katika jamii kwa kupata elimu ya kujikinga na maradhi na Huduma kwa Miradi ya Maendeleo Program ya kinga (**HH01010123)** ambapo vitaimarisha huduma za afya kwa kujengwa vituo vya Afya ya Msingi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati haikuridhishwa na suala la upatikanaji wa huduma za Mama na Mtoto kwani huduma zinazotolewa hazilingani na matarajio ya wananchi kwa kuwepo uhaba wa wahudumu na Madaktari katika Kitengo cha Uzazi, ni vyema Serikali kuliangalia suala la kuongeza Madaktari katika Kitengo hicho.

## PROGRAMU KUU YA TIBA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaunga mkono uwamuzi wa Serikali wa kuipatia Wizara Bajeti ya Shilingi Bilioni **64,552,050,000** katika Fungu **PH0102** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Binguni, Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi pamoja na Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Afya. Hivyo Kamati inaishauri Wizara kuwashirikisha Wataalamu katika Miradi husika ili kuepusha gharama za ziada katika utekelezaji wa Ujenzi wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwenye suala la Outsource katika upatikanaji wa huduma Hospitalini, Kamati imeona licha ya ugeni wa huduma hii hapa Zanzibar lakini kuna hatua kubwa ya maendeleo kwenye upatikanaji wa huduma za matibabu kama upatikanaji wa dawa, vipimo vya uhakika na kwa wakati. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua hii muhimu ambayo inakwenda kuimarisha huduma bora za Afya.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilihoji kuhusu Kifungu cha Huduma za Hospital za Vijiji, Wilaya na Hospital za Rufaa **(HH01020101)** kutokupangiwa Makadirio ya matumzi na kuarifiwa kuwa huduma za hospitali hizo zimewekezwa katika huduma za Outsource ambapo Kamati inaishauri Wizara kufuatilia kwa karibu upatikanaji wa huduma hizo ili Kampuni zilizopewa kazi hii ziweze kutoa huduma hizo kwa ufanisi sambamba na kuunda Bodi ya watumiaji kwa ajili ya kufanya tathmini ya upatikanaji wa huduma chini ya mpango huu wa outsource na kulinganisha na huduma kabla ya mpango huu pia tathmini hiyo izingatiye thamani ya fedha .

## PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA AFYA.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu **(PH0103)** imetengewa Shilingi Bilioni **39,883,789,000** sawa na asilimia 14 ya Bajeti ya Wizara ambapo miongoni mwa kazi zitakazotekelezwa ni: -

- Kupeleka masomoni Madaktari na Wafanyakazi wa kada nyengine za Afya.
- Kuimarisha mifumo endelevu ya kugharamia huduma za Afya.

- Kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa takwimu za Afya.
- Kufanya ufuatiliaji wa tathmini katika ngazi zote za utoaji huduma.

Kukamilika kwa vipaumbele hivyo itapelekea kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya na kupunguza msongamano katika sehemu za utoaji huduma Hospitalini.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilipata fursa ya kukagua kituo cha Afya cha Chake Chake Pemba na kubaini kuwa Mifumo ya utoaji wa Huduma iliyopo haifanyi kazi kutokana na kukosa Fedha za kuendeleza Mifumo hiyo na ukosefu wa Wataalamu wa IT. Kamati inaishauri Wizara kutafuta Wataalamu wa IT na kuweka bajeti ya kutosha kuhakikisha kuwa mifumo hiyo inakua endelevu kwa kuipitia na kuikagua mara kwa mara ili kujua changamoto zinazohusiana na mifumo hiyo na kuweza kuzitatua kwa haraka.

## FUNGU H02 HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

**Mheshimiwa Spika,**

Katika Kifungu PH0202, Programu Kuu ya uendeshaji na Uratibu wa Hospitali ya MnaziMmoja, Kamati imebaini kuwepo kwa ongezeko la kibajeti katika kifungu hicho na kuarifiwa kuwa imetokana na uwepo wa Mradi wa kukarabati na kupandisha hadhi Hospitali ya MnaziMmoja.

**Mheshimiwa Spika,**

Kuhusu uendeshaji wa Divisheni ya Afya ya Akili Hospitali ya Kidongo Chekundu, Kamati inaishauri Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuitengea fungu maalum la uendeshaji wa Divisheni hiyo na sio

vyema kutegemea fedha kwa asilimia kubwa kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya uendeshaji wa hospitali hiyo. Kamati imebaini kuwa kuna urasimu mkubwa unaopelekea watendaji katika hospitali hiyo kushindwa kutekeleza majukumu ya kazi kwa ufanisi kutokana na kuchelewa kupata mahitaji ya huduma muhimu za Hospitali mpaka huduma hizo zitolowe kupitia Hospitali ya Mnazimoja.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kifungu cha Mapato **H0202** Program Kuu ya Huduma za Uchunguzi na Matibabu, Wizara ilikadiriwa kukusanya Bilioni **1,090,400,000** katika mwaka ulipita. Kamati iliarifiwa kuwa mpaka kufikia Marchi 2024 makusanyo ya Wizara yalikuwa shilingi Milioni **306,000,000** katika huduma hiyo. Kamati ilihoji ongezeko kubwa la makadirio ya mapato ambapo yamekadiriwa kufikia Shilingi Milioni **930,886,000** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo Wizara imesema kuongezeka matarajio hayo kumetokana na uanzishwaji wa huduma ya Bima ya Afya.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaunga mkono jitihada za Serikali juu ya kuwapatia Wananchi Afya bora ambapo katika Bajeti ya 2024/2025 Serikali kupitia Mradi wa Kuimarisha huduma za afya kwa watu wasiojiweza na makundi maalumu katika jamii imepanga kuwapatia huduma za Bima wananchi. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha uwepo wa huduma zenye viwango na za wakati ili kufanya huduma hizo zilingane na malipo yanayofanyika.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho, napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena Viongozi na

Watendaji wa Wizara ya Afya kwa juhudi wanazozichukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano wao kwa Kamati hii. Vile vile, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa vile Kamati ya Ustawi wa Jamii imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako waijadili, watoe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimae waiunge mkono Bajeti hii ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya kusema hayo machache, Kwa niaba Kamati naunga mkono hoja.

**Mheshimiwa Spika,**
Naomba kuwasilisha.

………………………………………

Mhe. Sabiha Filfil Thani,
Mwenyekiti,
Kamati ya Ustawi wa Jamii,
**BARAZA LA WAWAKILISHI,**
**ZANZIBAR.**